# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,**

Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuamka salama na kuweza kufika hapa leo hii kuendelea na shughuli zetu za kulijenga taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inampongeza Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa tena kuendelea kushika wadhifa huu kwa kipindi chengine ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uteuzi wako ni uthibitisho wa imani aliyonayo Mheshimiwa Rais kwako katika utendaji wako uliotukuka, tunamuomba Mwenyezi Mungu akusimamie katika kumshauri vyema Mheshimwa Rais, ili hatimae Serikali yetu iweze kukamilisha ahadi zake kwa wananchi kama ilivyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto chini ya uongozi wake Mheshimiwa Waziri Anna Athanas Paul pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii, kwa juhudi zao wanazichukuwa katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za dhati pia nazishusha kwa wajumbe wa Kamati ambao muda wote walionesha umahiri wao katika kutekeleza majukumu ya kazi za Kamati. Wajumbe ambao walikuwa mstari wa mbele katika kumshauri vyema Mwenyekiti katika kufikia maamuzi pale ilipohitajika kufanya hivyo. Naomba niwatambuwe wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Dkt. Nasra Nassor Omar | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Issa Ussi Haji (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Seif Hamad Suleiman | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Shaame Ali Ali | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Zainab Khamis Shomari | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inafanya kazi kwa kushirikiana na Makatibu ambao kwa kweli muda wote wako karibu sana na Kamati katika kuipatia ushauri na miongozo inayofaa. Naomba niwatambuwe Makatibu hao kama ifuatavyo:

1. Ndugu Mussa Issa Mussa;
2. Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri; na
3. Ndugu Mohamed Raymond Mwellu (Afisa Bajeti).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilikaa na kupitia kwa kina Muelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Baraza La Wawakilishi inavyoelekeza, Kamati yangu imekubaliana na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na kubaini baadhi ya mapungufu ambayo iliishauri Wizara kuyafanyia marekebisho yanayofaa kwa lengo la kuboresha

utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi **Milioni 15,000,000** kupitia chanzo chake cha ukodishaji wa ukumbi wa Mikutano uliopo Sebleni, ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi 2026 Wizara ilikusanya shilingi **Milioni 9,200,000** sawa na **asilimia 61** ya Makadirio.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara, kwa kufikia kiwango kizuri cha ukusanyaji wa mapato na inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii kutafuta vyanzo vyengine ambavyo vitasaidia katika kuingiza fedha mbali ya hiki kilichopo kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuweka kizuia sauti (sound proof) katika ukumbi uliopo ndani ya Makaazi ya Wazee Sebleni, ili kuondosha kero kwa wazee wanaoishi humo hasa nyakati za usiku, ambapo muda huo ni wa mapumziko kwao na mara nyingi ndio muda ambapo muziki unapokuwa unapigwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ilitekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu, ambazo ni Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii, Programu Kuu ya Uratibu na Uendeshaji na Programu Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia, ambazo zote kwa pamoja zilikadiriwa kutumia shilingi **bilioni 17,084,260,000** na hadi kufikia mwezi Machi 2026 shilingi **bilioni 13,776,091,416** sawa na asilimia **81** ya Makadirio zilipatikana.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha utakaoishia Juni 2027, Programu hizi zimekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 26,648,026,056** ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali kwa ongezeko hilo, na kuiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia fedha hizo zote na kwa wakati, ili waweze kukamilisha malengo waliyojipangia.

**PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII**

Lengo la kuanzishwa kwa Programu hii ni kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, ili kupunguza kiwango cha umasikni nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga Nyumba za Makaazi ya Wazee visiwani Zanzibar kwa lengo la kuwapa hifadhi wazee wanaoishi katika mazingira mgumu na hatarishi. Kwa upande wa Unguja, nyumba hizi zimejengwa katika maeneo ya Sebleni na Welezo na Limbani kwa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imetumia fedha nyingi kwa ujenzi wa nyumba hizi, hivyo ni jukumu la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuzitunza nyumba, ili ziweze kubakia katika uhalisia wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilibaini katika ziara zake changamoto kubwa wanazopitia wazee wanaoishi katika makaazi ya muda, ***Limbani*** ambayo si rafiki hata kidogo kwa mustakabali mwema wa maisha yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hii kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuimarisha huduma zinazotolewa kwa wazee wanaoishi katika nyumba ziliopo Limbani, Sebleni na Welezo kwa lengo la kuimarisha ustawi wao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inawapongeza wahudumu wanaowashughulikia wazee katika Makaazi haya. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara hii kuwaangalia wahudumu hawa kwa kuwapa motisho zaidi, ili waweze kupata moyo na ari wa kuendelea kuwatunza wazee wanaoishi katika makaazi ya Serikali, kama tunavyojua wazee kufikia hatua hii ni sawa na hatua ya utoto kulingana na matendo yao kitabia. Sisi sote ni wazee watarajiwa, hivyo ni busara sana kuwaenzi, kuwatunza na kuwapatia huduma zote muhimu kulingana na mahitaji yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwaondolea Wazee katika Makaazi ya Sebleni changamoto ya ukosefu wa vyombo vya usafiri, kwa kuwapatia gari kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuitunza na kuisimamia gari hiyo na kuhakikisha inatumika kwa matumizi ya Wazee tu na si vyenginevyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umuhimu mkubwa wa huduma za uwendeshaji wa Pencheni Jamii kwa wazee nchini, Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuratibu mpango huu kwa wazee wenye umri wa miaka sabiini na kuendelea na kufanikiwa kuwasajili wazee 33,540 kwa Unguja na Pemba. Ni hatua nzuri ya maendeleo inayoonesha jinsi gani Serikali inavyowathamini na kuwaenzi wazee wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia hali hii Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuondosha urasimu na ubaguzi katika utekelezaji wa suala hili na kuhakikisha Wazee wote waliofikia umri huu wanasajiliwa na kupatiwa haki yao hii ya msingi.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali, kuongeza kiwango cha Pencheni kwa Wazee, ili kuwawezesha nao kuishi kulingana na gharama za maisha zinavyopanda siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inasikitika kuona fedha za Pencheni Jamii kulipwa na Wizara ya Fedha na Mipango, lakini uratibu wa shughuli hii unafanywa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inaishauri Serikali kwamba jukumu la kuratibu na kulipa fedha za Pencheni Jamii kwa wazee lirudishwe kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Suala la kuwaenzi wazee wetu haliishi katika Pencheni Jamii pekee, Wizara pia inadhamana ya kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yote hususani wale wenye mazingira magumu zaidi kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi zao. Hata hivyo, Kamati inatoa wito kwa jamii kuwahurumia pamoja na kuwapa kipaumbele wazee wetu katika sehemu za upatikanaji wa huduma kama vile benki, usafiri wa umma na hospitali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii imekadiriwa kutumia shilingi **bilioni 8,884,661,000** fedha ambayo imeongezeka ukilingaisha na fedha ya makadirio kwa mwaka **2025/2026** ambazo ni shilingi **bilioni 4,212,314,000.** Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha hii kwa wakati, ili waweze kutimiza vyema malengo waliyojipangia.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inasimamia masuala ya maendeleo ya jamii ikiwa ni pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, na utekelezaji wa haki za wanawake, wanaume na watoto.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara kupitia Programu hii inabeba jukumu zito na la msingi katika kuhakikisha hali za maisha ya wanajamii zinaimarika, makundi maalumu yanalindwa na hata kubadilisha mila kandamizi zinazoendelea kushika hatamu katika jamii siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Jamii, Usawa wa Kijinsia na Maendeleo ya Watoto ***S0202,*** utekelezaji wake unahitaji kupanga, kusimamia na kuunganisha shughuli zote zinazolenga kuinua hali za maisha ya wananchi. Waratibu wa wanawake na watoto wa Shehia ni kiungo muhimu katika kulikamilisha hili, waratibu ambao wanatekeleza maukumu yao katika mazingira magumu.

**Mheshimiwa Spika,**

Moja ya dhamana yao kubwa ni kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya udhalilishaji wa kijinsia unaoendelea katika jamii yetu siku hadi siku. Kazi kubwa wanayoifanya ya kutoa elimu juu ya kupunguza janga hili, haiwiani kabisa na malipo wanayolipwa kutoa Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiingizia Programu hii fedha yote iliyopangwa na kwa wakati, ili waratibu wa Shehia nao waweze kuimarishiwa maslahi yao, hali itakayowawezesha kufanya kazi kwa moyo na kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 10,743,631,000,** fedha ambayo ni kubwa ukilinganisha na fedha iliyokadiriwa kwa mwaka 2025/2026.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA UTAWALA

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ilikadiriwa kutumia shilingi **Bilioni 7,730,025,000** na hadi kufikia Machi 2026 ilifanikiwa kuingiziwa shilingi **bilioni 3,250,445,259** sawa na asilimia **54,** fedha ambayo imepungua ukilinganisha na fedha iliyokadiriwa kwa mwaka 2026/2027 ambayo ni shilingi **bilioni 7,037,890,000.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na umhimu mkubwa wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuingizia Programu hii fedha yote na kwa wakati, ili shughuli zilizopangwa ziweze kutekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitika sana kuiona Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hadi leo inatumia jengo la kukodi kama ofisi kwa gharama ya shilingi Milioni 26 kwa miezi mitatu (Quarter) ambayo ni sawa na shilingi **Milioni 8,600,000** kwa mwezi fedha ambayo ni kubwa kulinganisha na uhalisia wa jengo lilivyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kuirejeshea Wizara hii Ofisi yake iliyopo Mwanakwerekwe au iwajengee jengo jengine ambalo litaweza kukidhi mahitaji yao na kuondokana na usumbufu walionao hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika vyuo vilivyomo ndani na nje ya nchi, mafunzo ambayo yatawasaidia kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi yanayoendelea kutokea duniani kote.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati imebaini changamoto ya kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Ukarabati wa Nyumba za Makaazi ya Wazee Limbani, hali iliyopelekea wazee kuishi katika mazingira hatarishi. Wizara iliamua kuwakodia nyumba Wazee hao kupisha ukarabati huo, Nyumba hizo hazikuwa rafiki kwao hasa tukizingatia uhalisia wa nyumba zenyewe na uchafu uliozunguka nje na ndani ya jengo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo, Kamati ilimuagiza Mkandarasi wa Ujenzi kukamilisha haraka matengenezo yaliyobakia, ili wazee wetu waweze kuishi katika mazingira mazuri na salama.

**Mheshimiwa Spika,**

kutokukamilika kwa wakati wa mradi huu kumechangiwa na mashirikiano madogo yaliyokuwepo kati ya Mkandarasi wa Kampuni ya OSAJU, Mshauri Elekezi na watendaji wa wizara hii. Baadhi ya watendaji wa wizara hii walithubutu kuvunja mkataba wa ujenzi huu, ambapo ujenzi ulikwisha kufikia asilimia 93 na malipo yalikwishafanyika kwa asilimia 95 bila ya Mheshimiwa Waziri kuwa na taarifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa lengo la kuleta ustawi wa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali wakati wa kutangaza tenda za Miradi ya Ujenzi kuchagua Wakandarasi wenye sifa na vigezo vinavyofaa, ili kuhakikisha kwamba, Miradi inakamilika kwa wakati na inakidhi viwango vinavyotakiwa. Mradi huu uligharimu jumla ya shilingi Bilioni 2.2 na hadi Kamati inafika katika eneo la Mradi jumla ya shilingi bilioni 1.9 tayari zilikwishalipwa kwa Mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika,**

Mradi wa PAMOJA nao kwa upande wake, Kamati haikuridhika na utekelezaji wa Mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo fedha nyingi zilizotumika hazikuendana kabisa na uhalisia wa shughuli zilizotekelezwa. Jumla ya shilingi **bilioni 10,284,775,000** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na hadi kufikia Machi 2026 Wizara ilitumia jumla ya shilingi **milioni 685,858,000** kwa kuandaa miongozo ya utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya uzalishaji, kufanya mikutano ya jamii ya kuutambulisha mradi, kutayarisha nyaraka na hadibu rejea na kutafuta wataalamu elekezi wanaohitajika katika kutoa taaluma.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na Watoto kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Miradi iliyomo ndani ya Wizara yake, ili kubaini uhalisia wa shughuli zinazotekelezwa na fedha zinazotumika. Ni jukumu la Wizara kuhakikisha Miradi inayotekelezwa inawanufaisha moja kwa moja wananchi na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni imani yetu kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Serikali kwa ujumla itayachukuwa maoni na ushauri wa Kamati na kuyafanyia kazi, ili kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezeka vyema na kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii inawaomba wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, waichangie bajeti hii na kuipitisha ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri aweze kutekeleza majukumu aliyojipangia katika Wizara yake kwa mwaka huu mpya wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya wajumbe wa kamati yangu ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Ahsante,**

--------------------------------

Hussein Ibrahim Makungu,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**